# FISIMAJI– TUANZE

IOSF
INTERNATIONAL OTTER SURVIVAL FUND
www.otter.org

## TUANZE VIZURI NA RAHISI… FISIMAJI NI NINI?



Fisimaji ni Mamalia lakini ina maana gani?
Mamalia ni tofauti na Wanyama wengine kwa sababu:

- Wana manyoya
- Wanazaa
- Wananyonyesha Watoto wao
- Wana damu joto

Je! Unaweza kutaja aina nyingine nne za mamalia?

1. ………………….. 2. …………………. 3. …………………. 4. ………………….

**Mustelids ni jina la Kisayansi la familia ya mamalia kama chororo, fisi-maji, nyegere, melesi, kicheche na konje.**

Hivyo, sasa tunajua kuwa Fisimaji ni Mamalia, Wao ni familia ya mamalia inayoitwa Mustelids. Kuna aina nyingi za Mustelids kote duniani lakini hizi ni chache tu:



**Melesi/Nyegere**



**Chororo**



**Konje wa Ulaya**

## Ardhini au Majini?

Fisimaji ni muhimu na nadra kuonekana kwani wao nusu hutegemea maji. Lakini hiyo inamaanisha nini? Ni njia nzuri ya kusema kwamba wanaishi nchi kavu na majini. Fisimaji hutumia muda wake kuogelea, kukamata samaki na pia kukimbia nchi kavu . Maisha katika mazingira haya yanaweza kuwa magumu lakini kwa bahati nzuri Fisimaji hukabiliana kikamilifu na mazingira yao kama kupumua, kutumia milango ya fahamu, kukimbia haraka na kupata joto kwenye wanapokuwa majini na nchi kavu!




# Fisimaji– Msingi


Angalia picha chini– **Je! Unaweza kutaja vitu viwili muhimu juu ya kila mnyama vinavyomsaidia kuishi majini?**



Nyangumi



Seal



Fisimaji

Hiyo ni kitu gani humfanya Fisimaji awe tofauti na kumuwezesha kuishi nchi kavu na majini?

1. Wanyama wengine wa baharini, kama nyangumi na Seal, wana Ngozi yenye mafuta mengi ambayo huwapatia joto. Lakini kwa Fisimaji, hii itawafanya kuwa wazito sana na kushindwa kukimbia kwa haraka nchi kavu. Kwa hivyo, Fisimaji wana tabaka mbili za manyoya. Tabaka la nje ambalo huzuia maji na tabaka la ndani linalosaidia kutunza joto. Manyoya ya Fisimaji ni muhimu sana, kila wakati wanapotoka kwenye maji ya chumvi lazima wajisafishe katika maji safi ili kuweka manyoya katika ubora!
2. Fisimaji wana miguu yenye utando katikati ya vidole unaowasaidia kuogelea haraka na kwa ufanisi zaidi ndani ya maji. Ni kama sisi tunapofunga vidole kuogelea, lakini Fisimaji ana utandu wa kudumu!
3. Fisimaji wana mkia mkubwa wenye nguvu. Huwa kama usukani na kuwaongoza wakati wanaogelea ndani ya maji.
4. Fisimaji wana miili minyoofu. Hii huwasaidia kusafiri kwa urahisi ndani ya maji na nchi kavu
5. Fisimaji ana masikio, macho na pua ambavyo viko kwenye mstari. Hii inamaanisha kuwa wanaweza kukaa ndani ya maji lakini wanaweza kusikia, kuona na kunusa kila kitu.

**Unajua?**
**Fisimaji wa baharini wana manyoya mazito zaidi ya wanyama wote duniani. wana 150,000 kwa cm2. Hiyo ni kama kuwa na nywele 150,000 katika eneo lenye ukubwa wa kucha yako ya kidole!**



# Aina ya Fisimaji

IOSF
INTERNATIONAL OTTER SURVIVAL FUND
www.otter.org

Fisimaji wana majina tofauti katika lugha tofauti. Kwa mfano 'Fisimaji' kwa Kihispania ni 'nutria', Kifaransa ni 'loutre' na Kiwahili ni Fismaji. Jina la kisayansi (kwenye mabano) hutumiwa na kila mtu duniani kote hivyo kila mtu anajua nini unamaanisha unapotumia !



*Aonyx capensis*



*Lutra lutra*



*Aonyx congicus*



*Lontra felina*



*Pteronura brasiliensis*



*Lutra sumatrana*



*Enhydra lutris*



*Aonyx cinereus*



*Lontra provocax*


*Lontra longicaudis*



*Lontra canadensis*



*Hydrictus maculicollis*



*Lutrogale perspicillata*

Unajua?
Fisimaji wa Mtoni 50,000 Amerika Kaskazini wanauawa.

Kuna aina 13 za Fisimaji kote duniani. Wanaishi katika mabara yote Isipokuwa Australia na Antaktika! Ili kujua zaidi juu ya kila aina ya Fisimaji angalia ramani ya mtegemeano ya IOSF katika http://www.otter.org/Public/OtterMap.aspx




# Uchunguzi wa Fisimaji

IOSF INTERNATIONAL OTTER SURVIVAL FUND www.otter.org


Je, unataka kwenda kutafuta Fisimaji na kujua dalili za uwepo wao? Hizi ni Dondoo za kukusaidia kabla ya kuanza!

**Dalili/ Ishara za Awali ni rahisi-** Unaona Fisimaji! Je ni rahisi kuwaona? Tutakupa dondoo chache



**TAZAMA -** Macho, masikio na pua ya Fisimaji vyote viko katika usawa. Hivyo inamaanisha kuwa wanaweza kukaa ndani ya maji lakini bado wakawa na uwezo wa kuona, kusikia na kunusa. Wakati Fisimaji yuko ndani ya maji unachoweza kuona ni sehemu ndogo ya vichwa vyao na, mkia wao pia ikiwa na bahati!

**Mikia -** Wakati Fisimaji anazamia chini ya maji mkia wake ndio kitu cha mwisho kuonekana. Hii inafanya iwe rahisi kutofautisha kati ya Fisimaji na Mnyama mwingine





**NYUMA -** Wakati Fisimaji wanakimbia huonekana 'Nundu' nyuma ya migongo yao. Nundu na mkia huwafanya watambuliwe

**SIKILIZA -** Wakati Fisimaji wana watoto mara nyingi hutoa sauti kali ya "piiiiip" kuwasiliana.



Ni muhimu sana wakati unatazama Fisimaji kuweka UMBALI SALAMA kati yao na wewe. Kamwe usikaribie sana wanyama wa porini kwani wana kawaida ya kujitetea! Daima kumbuka kuwa HAUTAKIWI kusumbua wanyama wa porini!



# KUCHUNGUZA FISIMAJI

Ishara au dalili zinazofuata (sekondari) ni rahisi kupata na zinaweza kukusaidia ikiwa kuna Fisimaji wanaoishi karibu au jirani. Tuangalie ishara au dalili kadhaa zakufuata.



**KINYESI**

Kinyesi cha Fisimaji mara nyingi huwa na mabaki ya mifupa ya samaki na magamba ya kaa. Kawaida ni cheusi na mara nyingi hufanya nyasi zikue haraka na ziwe za kijani kibichi. Ikiwa unaona nyasi ndefu na kijani zimesimama kuliko zingine, angalia vizuri unaweza ona kinyesi chake! Kinyesi cha Fisimaji hutumika kama mbolea ya nyasi na inasaidia kukuza!
Fisimaji wanatumia kinyesi kuweka alama kuashiria maeneo muhimu na himaya zao. Daima fikiria viashiria vya uwepo wa Fisimaji kama kinyesi wakati unatafuta viasharia vingine, kama vile mapango/ shimo na mabwawa ya maji safi

**MAPANGO/ SHIMO**

Makazi ya Fisimaji ni mapango na mashimo. Wanapenda kuwa na Mapango na sehemu zingine za kupumzika kando au jirani na makazi yao. Tafuta kinyesi! Ikiwa umeona pango au shimo, ni muhimu usisumbue, tafadhali achana nayo.





**NYAYO**

Nyayo za Fisimaji zina vidole 5 na utando katikati ya vidole.

**MABWAWA YA MAJI.**


Tayari unajua umuhimu wa manyoya ya Fisimaji. Wanahitaji kuyatunza vizuri kwa ajili ya Joto na ili kuvutia kuangalia. Baada ya Fisimaji kuwa ndani ya maji ya chumvi baada ya kutoka lazima asafishe manyoya yake katika maji safi. Uweka kinyesi kama alama ya kumbukumbu kwenye mabwawa yao ya kujisafishia.



.

**NJIA ZA FISIMAJI**

Wakati Fisimaji wanapita kwenye nyasi utengeneza uwazi chini na uweka alama za vinyesi kila sehemu. Mara nyingi unaweza 'kujua uelekeo kwa kuunganisha vinyesi kwa kufuata uelekeo wa njia wanayopita.






# Kwanini Fisimaji ni muhimu?

IOSF® INTERNATIONAL OTTER SURVIVAL FUND
www.otter.org

Fisimaji ni wanyama wanaokula nyama ambao wako nafasi ya juu katika mzunguko au mlolongo wa chakula. Wanyama wote wanaunganishwa na kile kinachoitwa mzunguko au mlolongo wa chakula. Kila kiumbe kwenye mzunguko wa chakula hula na kupata nguvu kutoka kwa kiumbe kilicho chini yake. Mzunguko wa chakula umeunganishwa kuunda mtandao wa chakula.

**Fikiria chakula ulichokula jana jioni, kilikula nini? Je! Unaweza kutengeneza mlolongo wa chakula hapo juu? Tumia mwongozo wa mlolongo wa chakula wa Fisimaji wa Rasia hapa chini.**

Tuangalie umuhimu wa Fisimaji wa Urasia kwenye mlolongo wa chakula? Mishale inaonyesha nani anakula nini.




Hivyo, fikiria Fisimaji wasingekuwepo. Hii ingeathiri wanyama wote ambao wako chini yake kwenye mlolongo wa chakula. Fisimaji ni muhimu sana na hudumisha usawa wa mtegemeano wa chakula wa viumbe wote!

Uchafuzi wa mazingira, kama vile plastiki, unapoingia ndani ya maji hatakama Fisimaji hawatokula, Bado itakuwa imemuathiri Fisimaji? NDIYO - Kwa mfano, ikiwa planktoni alikula kipande kidogo cha Plastiki, na Gegereka akala Planktoni, Samaki wakala Gegereka kisha Fisimaji akala samaki - Plastiki hiyo sasa itakuwa ndani ya Fisimaji. Kama Gegereka hula planktoni wengi na Samaki hula Gegereka wengi, hii inamaanisha Fisimaji anapata plastiki nyingi. Hii ni sawa na kwetu sisi Binadamu - kwa sababu sisi pia tunakula samaki!



# Kwanini Fisimaji ni Muhimu?

IOSF INTERNATIONAL OTTER SURVIVAL FUND www.otter.org


**MAKAZI**

Fisimaji wanaishi katika makazi tofauti na wanahitaji mazingira safi na salama. Kwa kuwa Fisimaji hukaa ndani ya maji na nchi kavu wanaihitaji mazingira safi na yasiyokuwa na uchafuzi.

Ikiwa utawaona Fisimaji inamaanisha mazingira yote ya majini na nchi kavu yako safi na salama na kuna chakula cha kutosha! Hivyo ni ishara nzuri kwa aina zote za viumbe, pamoja na sisi binadamu!

**MPANGILIO**

Kila aina ya Fisimaji ukabiliana na mazingira kutoshea katika makazi yake na kile anachokula. Angalia mifano mitatu.




Eurasian otter

Fisimaji wa Urasia wana meno na kucha kali zinazowawezesha kukamata na kushikilia chakula chao. Hii uwasaidia kukamata chakula/ mawindo yanayoteleza.



Asian Small-clawed otter


Fisimaji wa Asia wadogo wenye kucha hutumia 'vidole' vyao kuhisi na kukamata chakula chao. Wanaweza kufika kwenye mashimo na kukamata mawindo yao.




Sea otter

Fisimaji wa baharini hutumia maisha yao mengi baharini na wana kiganja kikubwa kinachowasaidia kuogelea. Hii huwasaidia kushikilia chakula chao / windo na kuvunja gamba gumu akiwa juu ya jiwe analopenda.

Unafikiri ni mawindo/chakula kipi Fisimaji hula kati ya hivi?








________________ ________________ ________________



# Fisimaji anafurahisha!

IOSF
INTERNATIONAL OTTER SURVIVAL FUND
www.otter.org

Sasa ni zamu yako! Cheza michezo kadhaa na ujifunze zaidi juu ya Fisimaji na mazingira!!




**Uchafuzi wa mazingira** ni kitu kinachoathiri aina zote za viumbe hai. Angalia picha na zungushia duara vitu ambavyo unafikiri vinaweza kudhuru/ kuathiri wanyama, kama vile Fisimaji! Tumia nafasi iliyo hapo chini kuandika ni kwanini vitu hivi vinaweza kudhuru wanyama:



# Mfuko wa Kimataifa wa Kuokoa Fisimaji

Mfuko wa Kimataifa wa kuokoa Fisimaji (IOSF) umejitolea kulinda na kuhifadhi aina zote 13 za Fisimaji ulimwenguni! Hadi sasa imehusika sana katika miradi zaidi ya nchi 60 tofauti, pia na shughuli nyingine:



**HOSPITALI YA FISIMAJI** - IOSF inajali zaidi ya Fisimaji waliojeruhiwa na yatima zaidi ya 200, pamoja na wanyama wengine wa porini. Majeruhi wengi ni Watoto wa Fisimaji, yatima ambao hufika katika kituo kama watoto ambao ukuzwa na kulelewa mpaka wanakapokuwa tayari wakubwa kwa ajili ya kutolewa. Watoto wa Fisimaji hukaa na mama zao muda wa miezi 12-15 hivyo lazima wakae hadi umri huo na IOSF. Kulea Watoto wa Fisimaji ni gharama ni karibu paundi 1,600!
IOSF mara nyingi hufika maeneo mengi duniani kote Pamoja na washauri na wataalamu wetu juu ya kulea na kukuza Watoto wa Fisimaji. Mfuko umesaidia nchi tofauti ikiwa ni pamoja na Iraq, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Guyana.
**ELIMU** - Shida kubwa inayokabili Fisimaji duniani kote ni ukosefu wa ufahamu au uelewa. Tunatembelea shule na kutoa elimu ili kuongeza uelewa wa aina za Fisimaji na Maisha yao. Tumeunda kadi za kitambulisho cha Fisimaji ambazo zimetafsiriwa katika lugha tofauti tofauti.
Mtandao wetu mkubwa wa wafanyakazi na wanaojitolea husaidia kuelimisha jamii duniani kote kuhusu Fisimaji.
**MAFUNZO** - Mbali na ukosefu wa ufahamu/ uelewa kuhusu Fisimaji, pia hakuna utafiti wa kutosha uliofanyika duniani kuhusu Fisimaji. Tunaendesha semina za uhifadhi wa Fisimaji vijijini na kwa maafisa wa serikali mbinu za uhifadhi wa Fisimaji. Tumefanya Warsha 6 za Kimataifa pamoja na semina ya kwanza kubwa ya uhifadhi wa Fisimaji barani Afrika na 5 Asia. Warsha hizi za mafunzo zimeongeza mtandao wa Fisimaji duniani na kusaidiana kufanya kazi pamoja na kupashana habari duniani kote.
**UTAFITI** - IOSF inafanya utafiti hapa Uingereza na nje ya nchi.
Tunafuatilia idadi ya Fisimaji kwenye Kisiwa cha Skye kila mwaka, pamoja na lishe na idadi yao,hivyo tunaweza tambua kushuka kwa idadi yao.
Tunapeleka pia Fisimaji waliokufa katika Chuo Kikuu cha Cardiff kwa uchunguzi zaidi. Hii hutusaidia kujua ni muda gani Fisimaji wanaishi porini, sababu ya kifo na uchafuzi wowote ambao unaweza kuwa katika mazingira. Kutumia taarifa hizi tunaweza kushughulikia shida yoyote!
Tunasaidia na kufanya utafiti kote duniani. Kwa kutumia mtandao wetu mkubwa wa wafanyakazi na wanaojitolea kusaidia kuendelea na utafiti. Kwa mfano, mnamo mwaka 1998 Fisimaji wenye nywele puani waliaminika kutoweka! Mnamo mwaka 1999, mtoto mmoja wa Fisimaji alipatikana Kusini mwa Thailand. IOSF ilishughulikia tatizo na idadi yao kuongezeka kote Asia ya Kusini-Mashariki.
**KUPUNGUZA BIASHARA** - Iwe halali au haramu Fisimaji wanawindwa na hii lazima ikome! Kwa kawaida Seal huwindwa kwa ajili ya manyoya yao na kwa ajili kufugwa kama wanyama wa nyumbani mambo yote husababisha shida kubwa kwa Fisimaji! Katika maeneo mengine wametoweka. IOSF inapenda sana kupunguza biashara hii, biashara haramu na halali kisheria kwa nchi kama Marekani na Kanada.



# Ni namna gani unaweza saidia?

Fisimaji wanakabiliwa na shida mbalimbali kama: Uchafuzi wa mazingira, uwindaji, uharibifu wa makazi yao na mengine mengi. Tumia ukurasa huu kujifunza jinsi unavyoweza kusaidia Fisimaji na mazingira.

1. Tumia chupa za maji zinazoweza kutumika tena. Chupa za plastiki Zaidi ya MILIONI zinanunuliwa duniani kila DAKIKA! Tumia chupa za maji zinazoweza kutumika tena na ujaze maji kutoka kwenye bomba. Njia hii itapunguza uingiaji wa plastiki kwenye mazingira yetu!
2. **'BAHARI'** – Kampeni mpya duniani imeanza ya kuondoa plastiki katika mazingira yetu. Kila wakati watu utembea, huchukua vipande 3 vya plastiki nyumbani na kuviweka kwenye pipa za taka. Ikiwa kila mtu anafanya hivyo tutakuwa tumeleta mabadiliko makubwa.
3. **'FUNGA BOMBA** - Usiache bomba inamwaga maji. Kwa mfano, Baada ya kupiga mswaki! Dunia ina kikomo cha utoaji wa maji safi.
4. **ZIMA TAA -** Okoa Nishati! Tunatumia nishati nyingi kila siku, kwa kuzima taa tunapomaliza matumizi itasaidia kutunza mazingira.
5. **MTOTO WA FISIMAJI / MGOJWA AU MAJERUHI** - Ukiona mtoto wa Fisimaji unapaswa kufanya nini? kamwe usimchukue! Wakati mwingine mama anaweza kumwacha na kwenda kutafuta chakula na akarudi gafla ukiwa umemshika. Hivyo, anaweza kukung'ata. Mwambie mtu mzima anaweza kutazama na kujua, ikiwa hawana uhakika, piga simu muda wowote kwa **IOSF (+44) 01471 822 487**
6. **ENEZA HABARI NJEMA KUHUSU FISIMAJI**

**Fisimaji wanahitaji sauti yako!** Moja ya sababu kuu zinazowakabili Fisimaji Duniani ni ukosefu wa ufahamu/ uelewa juu ya uwepo wao.
Fisimaji hawawezi Zungumza - Hivyo tunahitaji kuzungumza kwa niaba yao! Tumia taarifa zote uliyojifunza na uwaambie rafiki zako juu ya habari njema, familia na kila mtu jinsi unavyomfahamu Fisimaji, na mafanikio ya IOSF katika kutunza Fisimaji.

**TIMU YA FISIMAJI**

Fuatilia ukurasa wa IOSF ukurasi wa watoto. Hapa unaweza kupata taarifa mpya, mashindano, michezo na maswali; www.loveotters.org

**IOSF**

Saidia kazi za IOSF! Kuna maoni mengi mazuri na ya kufurahisha kwenye tovuti yetu ambayo itakueleza jinsi unavyoweza saidia fisimaji www.otter.org



IOSF
INTERNATIONAL OTTER SURVIVAL FUND
www.otter.org

First produced in 2018
International Otter Survival Fund
7 Black Park
Broadford
Isle of Skye
IV49 9DE
Email: enquiries@otter.org
Website: www.otter.org
Phone: +44(0) 1471 822 487
Charity Number: SC003875

Text Copyright ©International Otter Survival Fund 2018
Image Copyright ©Lyn Wells
© Mike Matthews – A Call for Nature
All photographs copyrights © to individual photographers as listed

All rights reserved by IOSF. This publication is free for use for educational purposes but for any other use please contact IOSF beforehand.

**Acknowledgements**

Thank you to William Mgomo for translating this pack

**©International Otter Survival Fund 2018**

